TANGAZO LA SERIKALI Na. 361 la tarehe 19/5/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 9(1)(a))*

NOTISI YA KUANZISHA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA SIMIYU YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kuanzisha Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Simiyu ya Mwaka 2023

Kuanzisha Mamlaka ya Maji

2. (1) Maeneo yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii yanatangazwa kuwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira.

(2) Mamlaka itakuwa na jukumu la kusimamia na kuendesha miundombinu ya maji inayoimiliki na kusambaza maji kwa ujumla kwa -

(a) Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira;
(b) Vyombo vya kijamii; na
(c) Vijiji vilivyopo katika eneo lake la huduma.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2(1))*

| | JINA LA MAMLKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA | ENEO LA HUDUMA |
|---|---|---|
| | Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Simiyu | Water Intake at Ziwa Victoria, Wilaya ya Busega, Wilaya ya Bariadi, Wilaya ya Itilima, Wilaya ya Maswa, Wilaya ya Meatu na Vijiji vilivyopo karibu na bomba kuu. |

Dodoma
…………….., 2023

JUMAA H. AWESO,
*Waziri wa Maji*